JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

Simu No. 025 2552357

Fax: 025 2552357
Mob: 0789663336/0713153162
0754777743
Email: tukuyutc@moe.go.tz

CHUO CHA UALIMU TUKUYU,
S. L. P. 554,
TUKUYU.

Kumb.Na.CCU/TKY/MGT/VOL.VIII/ **Tarehe : 02 Julai, 2020**

Ndugu ……..

……

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA UALIMU NGAZI YA DIPLOMA KWA MWAKA 2020/2021

1. Utangulizi

Ninafurahi kukujulisha kwamba umechaguliwa na **Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia** kwa kushirikiana na**Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa**(**OR – TAMISEMI)**kujiunga na mafunzo ya Ualimu ngazi ya **STASHAHADA (DIPLOMA)**katika chuo hiki kwa mwaka wa masomo **2020/2021.***Ninakupongeza sana!*

Moto wa Chuo chetu ni **ELIMU NI KAZI.**

1.2 Mahali Chuo Kilipo

Chuo cha Ualimu Tukuyu kipo mkoani Mbeya, wilaya ya Rungwe, umbali wa ***km 70*** kutoka Mbeya Mjini. Chuo kipoTukuyu Mjini, mtaa wa Msasani umbali wa ***km 2*** kutoka stendi kuu ya mabasi ya **TUKUYU.** Hali ya hewa ni ya baridi na mvua za mara kwa mara karibu mwaka mzima.

1.3 Kuripoti Chuoni

Unatakiwa kuripoti chuoni **tarehe 24.08.2020 bila kukosa** ili kuhudhuria mafunzo kabilishi ***(Orientation Course)*** yatakayoanza mara moja. Mwisho wa kuripoti chuoni ni tarehe **07/09/2020**. Iwapo utachelewa hutapokelewa na nafasi yako atapewa mtu mwingine.

1.4 Mafunzo Yatolewayo Chuoni

Chuo kinatoa mafunzo ya Ualimu **STASHAHADA MAALUMU YA SAYANSI, HISABATI na TEHAMA (SPECIAL DIPLOMA IN SCIENCE, MATHEMATICS ANDICT)**. Kila mwanachuo atasoma masomo kama alivyopangiwa na Wizara na masomo mengine ya Ualimu/Utaalamu. Maelezo zaidi yatatolewa wakati wa mafunzo kabilishi.

Katika kipindi chote cha mafunzo, kila mwanachuo atatakiwa kufaulu mazoezi ya darasani na mitihani mbalimbali itakayotolewa.

2. MAHITAJI KWA AJILI YA USAJILI

Unatakiwa kuja na Vitu/Vitambulisho vifuatavyo ambavyo utavionyesha wakati wa usajili;

VYETI NA VITAMBULISHO

- Barua hii ya kuitwa chuoni
- Cheti cha kuzaliwa
- Vyeti **halisi** vya kidato cha **IV(Academic&LeavingCertificates)** na vyeti vingine ulivyosomea na vivuli vyake, nakala tatu kila kimoja .
- Kitambulisho chochote chenye picha na jina lako (mf. cha Mpiga kura)

a. **ADA**

Ada yaMafunzo ni **Tshs.450,000.00**kwa mwaka. Fedha hizi zitalipwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali baada ya kutengenezwa **Control Namber**ya kulipia hapa chuoni.

b. **MICHANGO**

i. Huduma ya kwanza (matibabu) **Tshs. 10,000.00**kwa muhula.
ii. Usajili na kitambulisho **Tshs 20,000.00** inalipwa mara mojamwaka wa kwanza
iii. Serikali ya Wanachuo**Tshs. 5,000.00**kwa mwaka
iv. Kukodi godoro**Tshs 10,000.00**kwa muhula.
v. Ukarabati **Tshs. 25,000.00**(kwa mwaka)
vi. Elimu ya Michezo **Tshs 30,000.00**kwa mwaka.
vii. Ulinzi **Tshs 30,000.00** kwa mwaka
viii. Usafi, mazingira na elimu yakujitegemea **Tshs. 20,000.00**kwa mwaka
ix. Gharama za mahafali mtajulishwa mwaka wa mahafali.

JUMLA YA MICHANGO SHILINGI 150,000.00

NB: UTARATIBU WA MAFUNZO KWA VITENDO PAMOJA NA GHARAMA ZAKE UTAUPATA UFIKAPO CHUONI

Muhimu:

(i) ***Fedha za michango mingine*** zilipwe benki ya ***NMB*** (Tukuyu TC General**A/C No. 6141000011*)***

(ii) Uje na ***Pay-in –Slip Original*** (**Siyo photocopy)** ikionesha kiasi kilicholipwa na yenye jina lako kamili.

(iii) Usichanganye akaunti, wala fedha yako ya matumizi isiwekwe katika akaunti hizo.

(iv) **FEDHA TASLIMU HAITAPOKELEWA!**

c. **Ream moja A4 ya karatasi 500 nyeupe kwa mwaka**

3. SARE

Wanaume

- **Suti** rangi ya bluu nyeusi **(darkblue)** angalia sampuli ya kitambaa (Suruali mbili na koti).
- Mashati mawili meupe ya mikono mirefu
- Viatu vyeusi vya ngozi vya kamba na vya kufunika na soksi nyeusi
- Tai ndefu inayofanana na rangi ya suruali.
- Koti jeupe la maabara.

Wanawake

- Suti rangi ya bluu nyeusi **(darkblue)** angalia sampuli ya kitambaa (sketi mbili na koti)
- Mshono wa sketi uwe ni wa **solo isiyobana** yenye urefu wa sentimita 12 chini ya magoti.
- Mashati mawili meupe ya mikono mirefu.
- Viatu vyeusi vya kufunika, vya kamba na vyenye visigino vifupi na Soksi nyeupe.
- Skafu inayofana na rangi ya sketi.
- Koti jeupe la maabara
- **Kwa watakaovaa Hijab**: ivaliwe nusu kanzu nyeupe nzito, isiwe nyepesi (transparent), ushungi mweupe na koti la rangi ya bluu nyeusi **(darkblue).**
  (kwa mashono ya sare angalia ilivyo katika michoro na 1 & 2 zifuatazo)

NB Sare (Suti) ya Chuo unaweza kushona ufikapo chuoni.

PICHA 1 **PICHA 2**

4. MAVAZI MENGINE MUHIMU

i. Mavazi kwa ajili ya Michezo

- **Track Suit** nyeusi au bluu nyeusi(darkblue)
- Raba nyeupe na soksi zake
- T-shirt rangi nyekundu au njano (isiwe na maandishi)
- **T – Shirt yenye Nembo ya Chuo Tshs. 15,000.00 inapatikana chuoni**

ii.**Mavazi mengine.**

Kwa wakati mwingine wowote utatakiwa kuvaa mavazi ya heshima na yenye maadili ya kiualimu. **Mavazi ya kubana, jeans, kaptura (pensi) vimini, vitop na mavazi ya kufanana na hayo hayaruhusiwi.**

5. MAHITAJI MUHIMU KWA AJILI YA MALAZI

- Blanketi moja na shuka mbili (nyeupe), mto na foronya (nyeupe).
- Vyombo vya kulia chakula na ndoo.
- Dumu la kuhifadhia maji ya kunywa.

6. MAHITAJI YA LAZIMA KWA AJILI YA TAALUMA

- Madaftari makubwa ya kutosha (masomo kumi)
- Majalada matupu (flat files) kwa ajili ya mkoba wa kazi (Portifolio) kwa kila somo.
- Mihutasari miwili ya shule ya sekondari kwa masomo yako ya mchepuo.
- Vitabu viwili vya kiada (text books) kwa masomo yako ya mchepuo.
- Mathematical set na koti jeupe la maabara.

7. MAAGIZO MUHIMU KWA AJILI YA AFYA YA MWANACHUO

Unatakiwa kuzingatia yafuatayo kwa ajili ya ustawi wa afya yako kwa kipindi chote cha mafunzo :-

Uje na fomu ya afya (iliyoambatanishwa) ikiwa imejazwa kikamilifu na mganga wa hospitali /kituo cha afya kinachotambuliwa na serikali, ili kuthibitisha hali ya afya yako.

- Kwa wenye matatizo /mahitaji maalumu uje na uthibitisho wa daktari. **NB : Chuo hakitoi chakula maalumu (Special diet)**
- Uje na kadi ya **Bima ya Afya** kwa ajili ya matibabu yako yote. Chuo kinatoa huduma ya kwanza tu.
- Kwa wale ambao hawana Bima ya Afya watapaswa kujiunga na **Mpango wa bima ya afya kwa gharama ya tsh 50,400.00 kwa mwaka inayotolewa na Bima ya Afya ya Taifa.**

8. MWISHO:

Ualimu bora huanzia chuoni, hivyo, baada ya kusajiliwa utapitishwa katika Sheria na ***Kanuni za Mwenendo Bora wa Mwanachuo***ambapo utatakiwa kujaza fomu maalum kuthibitisha kuwa utazifuata wakati wote wa mafunzo.

Kwa mawasiliano zaidi tumia namba za simu zilizoonyeshwa hapo juu.

Karibu sana!

……

Ubaya S. Suleiman

MKUU WA CHUO

NAKALA:

1. Katibu Mkuu,
   Wizara ya Elimu, Sayansi naTeknolojia,
   Mji wa Serikali, Eneo la Mtumba,
   Mtaa wa Afya,
   S.L.P 10,
   40479 DODOMA.

2. Mthibiti Ubora wa Shule
   Kanda ya Nyanda za Juu
   S.L.P 92,
   MBEYA.
   Mwenyekiti wa bodi ya ushauri ya chuo
   S.L.P 993
   MBEYA

GOVERNMENT OF TANZANIA

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

PART A:

TO: The Medical Officer
Tukuyu Teachers' College.

From: Principal

P.O. BOX 554, TUKUYU

…….

…….

Please examine the above named as to his/her physical and mental fitness for a full time teachers course.

A: 1. (a) Eye – sight
(b) Hearing
(c) Speech
(d) Venereal Diseases
(e) Leprosy
(f) Limbs
(g) Epilepsy

2.Neuroses

3.Other serious diseases.

B: Blood Group

Date : …….. Signature……

Official Stamp

****

PART B: **MEDICAL CERTIFICATE.**

(To be completed by Government Medical Officer)

I have examined the above named student that he/she is physically fit/unfit and mentally *fit/unfit for a full time teacher Education course.

- (a) Eye – sight……
  (b) Hearing……...
  (c) Limbs……
  (d) Speech…….
  (e) Leprosy…….

II. Neuroses……

III. Other serious diseases……..

IV. pregnancy……..

Date:……..Signature……

Official Stamp